

DOLA BILIONI 3.1>>

Kibano wenye mabasi yasiyogeshwa Magufuli

Na EMMANUEL MOHAMED

WAMILIKI wa mabasi yaendayo mikoani yasiyo na vibali vya kugesha katika vituo vya Shekilango mkoani Dar es Salaam, wametakiwa kuyahamishia Stendi Kuu ya Magufuli mara moja.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkuu wa mkoa huo, Albert Chalamila alisema kumekuwa na mtindo wa baadhi ya mabasi kushusha na kupakia abiria katika maeneo hayo kinyume na sheria.

"Kuna stendi kubwa sana Wilaya ya Ubungo eneo la Mbezi, ambayo imejengwa kwa gharama ya zaidi shilingi bilioni 50, ambapo ina uwezo wa kuchukua magari mengi lakini kwa bahati mbaya sana hayapo pale," alisema Chalamila.

Alisema magari hayo yamekuwa yakizagaa Shekilango hadi barabara inayokwenda Magomeni wakati ni mabasi ya kampuni sita yaliyopewa na Mamlaka ya Udhambi Usafiri Ardhi (LATRA) kibali cha kufanya hivyo.

Mkuu huyo wa mkoa alisema kibali hicho kiliziruhusu kampuni hizo kujenga stendi ndogo katika maeneo ya Manzese na sehemu nyingine.

"Kwa kampuni nyingine zote ambazo hazina vibali ninazitaka zipeleke mabasi katika stendi ya Magufuli kuanzia leo (jana) hadi kufikia Agosti 17, mwaka huu," alieleza.

Aliagiza kampuni za mabasi hayo kuboresha huduma kwa kuanza kutumia mabasi madogo kubeba abiria kutoka katika stendi zao na kuwapeleka Mbezi kwa safari za mikoani.

Chalamila alisema kitendo cha kampuni hizo kuingiza mabasi katikati ya mji ni kusababisha foleni zisizo za msingi.

"Jambo lingine kampuni hizo zinanyang'anya fursa za waendesha pikipiki, bajaji, daladala na mabasi ya mwendokasi... bahati nzuri mabasi ya mwendokasi tumeyaunganisha na stendi ya Magufuli, kwa hiyo magari ya mikoani yanatakiwa kuishia Mbezi kuwezesha mabasi madogo kupata abiria," alisema.

Mkuu huyo wa mkoa aliagiza kuanzia jana mabasi yote yaliyogeshwa Shekilango yapelekwe stendi ya Magufuli kama taratibu inavyozitaka.

Aliisisitiza LATRA kutowapa vibali vingine kampuni ambazo vimekwisha muda wake, lengo mabasi yote yaanze safari stendi ya Magufuli.

Chalamila alisema pia Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ametoa fedha za ujenzi wa stendi kubwa upande wa Temeke ambayo itakuwa inahudumia abiria kutoka Kanda ya Kusini.

"Pia sasa tunaangalia uwezekano wa kuwa na stendi upande wa Bunju kuwahudumia abiria wanaotoka njia ya Bagamoyo na stendi hizi hazitakuwa sawa na stendi ya Magufuli," alisema.

MMILIKI AZUNGUMZA

Mmiliki wa mabasi ya Kampuni ya ERERA, Frolence Kilumanga, alisema uamuzi umetolewa ghafla kutokana na kampuni nyingi zenye ofisi Shekilango zimefanya uwekezaji mkubwa.

"Tumeingia mkataba wa kupangisha eneo la Urafiki, hivyo kinachotakiwa ni serikali kukaa na wadau kujua namna ya kuendesha shughuli zetu," alisema.

Aliongeza: "Tukisema mabasi yote tupeleke stendi ya Magufuli itakuwa ngumu kutokana na kampuni nyingine zina mabasi mengi yakipeleka pale patakuwa hapatoshi kabisa."

WAMILIKI SILAHA

Katika hatua nyingine, Chalamila aliwataka watu wote wanaomiliki silaha kisheria au kinyume cha sheria, kuzipeleka kuhakikiwa kuanzia Agosti 11 hadi 30, mwaka huu.

"Kuna wengine wamefiwa na ndugu zao waliokuwa wakimiliki silaha hizo, wahakikishe wakati michakato ya kurithi inaendelea wanaziwasilisha Jeshi la Polisi," aliagiza Chalamila.